# Microsoft License Terms

**Ilisasishwa Mwisho Desemba 2016**

**MASHARTI YA LESENI YA PROGRAMU YA MICROSOFT**

**MFUMO WA UENDESHAJI WA WINDOWS**

---

**IKIWA UNAISHI (AU IKIWA MAKAO YAKO MAKUU YA BIASHAYA YAKO) NCHINI MAREKANI, TAFADHALI SOMA KIFUNGU CHA USULUHISHI UNAOFUNGA NA MSAMAHA WA HATUA YA PAMOJA KATIKA SEHEMU YA 10. HUATHIRI JINSI MIZOZO HUTATULIWA.**

**Asante kwa kuchagua Microsoft!**

Kulingana na jinsi ulivyopata programu ya Windows, haya ni makubaliano ya leseni kati ya (i) wewe na mtengenezaji wa kifaa au msakinishaji wa programu ambaye husambaza programu pamoja na kifaa chako; au (ii) wewe na Shirika la Microsoft (au, kulingana na mahali unapoishi au ikiwa ni biashara mahali makao yako makuu ya biashara yako, mmoja wa washiraka wake) ikiwa umepata programu kutoka kwa muuzaji rejareja. Microsoft ni mtengenezaji wa kifaa kwa vifaa vilivyotengenezwa na Microsoft au mmoja wa washirika wake, na Microsoft ni muuzaji rejareja ikiwa ulipata programu moja kwa moja kutoka kwa Microsoft.

Mkataba huu unafafanua haki zako na hali ambazo unaweza kutumia programu hii ya Windows. Unastahili kuhakiki makubaliano yote, ikiwa ni pamoja na masharti ya ziada ya leseni ambayo yako pamoja na programu na masharti yoyote yaliyounganishwa, kwa sababu masharti yoye ni muhimu na kwa pamoja yanaunda makubaliano haya ya kisheria ambayo yayatumika kwako. Unaweza kuhakiki masharti yaliyounganishwa kwa kubandika kiungo cha (aka.ms/) kwenye dirisha la kivinjari.

**Kwa kukubali makubaliano haya au kwa kutumia programu, unakubaliana na masharti haya yote ya matumizi, na unatoa kibali kwa upitishaji wa maelezo mengine wakati wa uamilishaji na wakati wa matumizi yako ya programu kulingana na taarifa ya faragha iliyofafanuliwa katika Sehemu ya 3. Ukikosa kukubali na kufuata masharti haya, huenda usiweze kutumia programu au vipengele vyake.** Unaweza kuwasiliana na mtengenezaji wa au msakinishaji wa kifaa, au muuzaji wako rejareja ikiwa ulinunua programu moja kwa moja ili kubainisha sera ya urejeshaji na kurejesha programu au kifaa ili kufidiwa au mkopo chini ya sera hiyo. Lazima uafikiane na sera hiyo, ambayo huenda ikakuhitaji urejeshe programu na kifaa chote ambacho programu imesakinishwa ili kufidiwa au kupata mkopo, ikiwa upo.

**1. Muhtasari.**

**a. Sheria husika.** Makubaliano haya hutumika kwa programu ya Windows ambayo imesakinishwa mapema kwenye kifaa chako, au kupatikana kutoka kwa muuzaji rejareja na kusakinishwa na wewe, chombo ambacho ulipokea programu hiyo (ikiwa kipo), fonti zozote, ikoni, picha au faili za sauti zilizojumuishwa na programu, na hata pia visasisho vyovyote vya Microsoft, matoleo mapya, vya ziada au huduma za programu, isipokuwa masharti mengine yawe yanakuja pamoja. Hutumika pia kwenye programu za Windows zilizobuniwa na Microsoft ambazo hutoa utendaji kama vile barua, waasiliani, muziki na picha ambazo zimejumuishwa na ni sehemu ya Windows. Ikiwa makubaliano haya yana masharti yanayohusiana na kipengele au huduma ambayo haipatikani kwenye kifaa chako, basi masharti hayo hayatumiki.

**b. Masharti ya ziada.** Masharti ya ziada ya Microsoft na wahusika wengine yanaweza kutumika kwa matumizi yako ya vipengele, huduma na programu nyingine, kulingana na uwezo wa kifaa chako, jinsi kilivyosanidiwa, na jinsi unavyokitumia. Tafadhali hakikisha umeyasome.

(i) Baadhi ya programu za Windows hutoa eneo la ufikiaji kwa, au hutegemea, huduma za mtandaoni, na matumizi ya huduma hizo wakati mwingine husimamiwa na masharti ya kando na sera za faragha, kama vile Makubaliano ya Huduma za Microsoft kwenye (aka.ms/msa). Unaweza kutazama masharti na sera hizi kwa kuangalia masharti ya matumizi ya huduma au mipangilio ya programu, kama inavyotumika. Huenda huduma zisipatikane katika maeneo yote.

(ii) Microsoft, mtengenezaji au msakinishaji anaweza kujumuisha programu za ziada, ambazo hutegemea masharti ya kando ya leseni na sera za faragha.

(iii) Programu hujumuisha Adobe Flash Player ambayo ina leseni chini ya masharti kutoka kwa Adobe Systems Incorporated kwenye (aka.ms/adobeflash). Adobe na Flash ni alama za biashara zilizosajiliwa au alama za biashara za Adobe Systems Incorporated nchini Marekani na/au nchi zingine.

(iv) Huenda programu ikajumuisha programu za wahusika wengine ambazo umepewa leseni chini ya makubaliano haya, au chini ya masharti yake. Masharti ya leseni, ilani na ukubalifu, ikiwa ipo, kwa programu za wahusika wengine inaweza kutazamwa kwenye (aka.ms/thirdpartynotices).

(v) Kwa umbali uliojumuishwa na Windows, Word, Excel, PowerPoint na OneNote zina leseni za matumizi yako ya kibinafsi, yasio ya kibiashara, isipokuwa uwe una haki za kibiashara chini ya makubaliano mengine na Microsoft.

**2. Usanidi na Haki za Matumizi.**

**a. Leseni.** Programu ina leseni, haiuzwi. Chini ya makubaliano haya, tunakupa haki ya kusakinisha na kuendesha tukio moja la programu kwenye kifaa chako (kifaa chenye

leseni, kwa matumizi ya mtu mmoja kwa wakati mmoja, bora uafikiane na masharti yote katika makubaliano haya. Kusasisha au kuboresha kutoka kwa nakala isiyo halali kwa programu kutoka Microsoft au vyanzo vilivyoidhinishwa hakufanyi toleo lako halisi au lililosasishwa/kuboreshwa kuwa toleo halali, na katika hali hiyo, huna kibali cha kutumia programu.

**b.Kifaa.** Katika makubaliano haya, “kifaa” humaanisha mfumo wa maunzi (uwe halisi au pepe) wenye kifaa cha hifadhi cha ndani kinachoweza kuendesha programu. Sehemu au vipande vya maunzi vinachukuliwa kuwa kifaa.

**c.Vizuizi.** Mtengenezaji au msakinishaji na Microsoft wana haki zote (kama vile haki chini ya sheria za mali ya akili) zisizotolewa moja kwa moja katika makubaliano haya. Kwa mfano, leseni hii haikupi haki yoyote, na huenda usiweze:

(i) kutumia au kuiga vipengele vya programu kivyake;

(ii) kuchapisha, kunakili (kando na nakala iliyoruhusiwa ya chelezo), kukodisha, kupangisha, au kuazima programu;

(iii) kuhamisha programu (isipokuwa kama inavyoruhishwa na makubaliano haya);

(iv) kujaribu njia nyingine zilizozuiwa au vikwazo vya kiufundi katika programu;

(v) tumia programu kama programu ya seva, kwa upangishaji wa kibiashara, fanya programu ipatikane ili itumiwe kwa wakati mmoja na watumiaji wengi kwenye mtandao, sakinisha programu kwenye seva na uwaruhusu watumiaji kuifikia kwa mbali, au sakinisha programu kwenye kifaa ili itumiwe na watumiaji wa mbali tu;

(vi) ubadilishaji uhandisi, usimbuaji, au kuharibu programu, au kujaribu kufanya hivyo, isipokuwa iwe tu kwamba kizuizi hicho (a) kinaruhusiwa na sheria husika; (b) kinaruhusiwa na masharti ya leseni yanayosimamia matumizi ya vijenzi huria ambavyo vinaweza kujumuishwa na programu; au (c) inahitajika ili kutatua mabadiliko kwenye maktaba yoyote yenye leseni chini ya Leseni Ndogo ya Jumla ya Umma ya GNU (GNU Lesser General Public License) ambayo yamejumuishwa na kuunganishwa na programu; na

(vii) wakati unatumia vipengele vinavyotegemea intaneti, huwezi kutumia vipengele hivyo kwa njia ambayo itatatiza matumizi ya mtu mwingine, au kujaribu kufikia huduma yoyote au kutumia data, akaunti au mtandao wowote, kwa njia isiyoidhinishwa.

**d. Hali ya matumizi anuwai.**

(i) **Matoleo kadhaa.** Ikiwa wakati unapata programu ulipewa matoleo kadhaa (kama vile matoleo ya biti-32 na biti-64), unaweza kusakinisha na kuamilisha moja kati ya

matoleo hayo kwa wakati mmoja.

(ii) **Miunganisho ya ubia au kadhaa.** Maunzi au programu hutumia miunganisho anuwai au iliyojumuishwa, au hupunguza idadi ya vifaa au watumiaji ambao wanaweza kufikia au kutumia programu, haipunguzi idadi ya leseni unazohitaji. Huenda ukatumia maunzi au programu kama hiyo ikiwa una leseni kwa kila tukio la programu unayotumia.

(iii) **Miunganisho ya Vifaa.** Unaweza kuruhusu hadi vifaa vingine 20 kufikia programu iliyosakinishwa kwenye kifaa chenye leseni kwa lengo la kutumia vipengele vifuatavyo vya programu: huduma za faili, huduma za kuchapisha, huduma za maelezo ya Intaneti, na muunganisho wa Intaneti, huduma za kushiriki na simu kwenye kifaa chenye leseni. Unaweza kuruhusu kiwango chochote cha vifaa kufikia programu kwenye kifaa chenye leseni ili kulandanisha data kati ya vifaa. Hata hivyo, sehemu hii haimaanishi kwamba una haki ya kusakinisha programu, au kutumia kitendaji msingi cha programu (kando na vipengele vilivyoorodheshwa katika sehemu hii) kwenye vifaa hivi vingine.

(iv) **Matumizi katika mazingira pepe.** Leseni hii hukuruhusu kusakinisha tukio moja tu la programu kwa matumizi kwenye kifaa kimoja, iwe kifaa hicho ni halisi au pepe. Ikiwa unataka kutumia programu kwenye zaidi ya kifaa pepe kimoja, lazima upate leseni tofauti kwa kila tukio.

(v) **Ufikiaji wa mbali.** Bila kuzidisha mara moja kwa siku 90, unaweza kumteua mtumiaji mmoja ambaye hutumia kifaa halisi chenye leseni kama mtumiaji mwenye leseni. mtumiaji mwenye leseni anaweza kufikia kifaa chenye leseni kutoka kwa kifaa kingine kwa kutumia teknolojia ya ufikiaji wa mbali. Watumiaji wengine, kwa wakati tofauti, wanaweza kutumia kifaa chenye leseni kutoka kwa kifaa kingine kwa kutumia teknolojia za ufikiaji wa mbali, lakini kwenye vifaa vyenye leseni ya kando ili kuendesha toleo sawa au la juu la programu hii.

(vi) **Usaidizi wa mbali.** Unaweza kutumia teknolojia za usaidizi wa mbali kushiriki kikao kinachoendelea bila kupata leseni yoyote ya ziada ya programu. Usaidizi wa Mbali huruhusu mtumiaji mmoja kuunganisha moja kwa moja kwenye kompyuta ya mtumiaji mwingine, kwa kawaida kusahihisha matatizo.

**e.Nakala chelezo.** Unaweza kutengeneza nakala moja ya programu kwa malengo ya chelezo, na unaweza pia kutumia nakala chelezo kuhamisha programu ikiwa inahitaji na programu huru, kama ilivyofafanulia katika Sehemu ya 4 hapa chini.

**3. Faragha; Kibali cha Kutumia Data.** Faragha yako ni muhimu kwetu. Baadhi ya vipengele vya programu hutuma au kupokea maelezo wakati unatumia vipengele hivyo. Nyingi kati ya vipengele hivi vinaweza kuzimwa katika kiolesura cha mtumiaji, au unaweza kuchagua

kutovitumia. Kwa kukubali masharti haya na kutumia programu unakubali kwamba huenda Microsoft ikakusanya, ikatumia na ikafichua maelezo kama ilivyofafanuliwa katika Taarifa ya Faragha ya Microsoft (aka.ms/privacy), na kama inavyoweza kufafanuliwa katika kiolesura cha mtumiaji chenye vipengele vya programu.

4. **Uhamishaji.** Matoleo ya sehemu hii hayatumiki ikiwa ulipata programu kama mtumiaji nchini Ujerumani au katika nchi yoyote iliyoorodheshwa kwenye tovuti hii (aka.ms/transfer), katika hali hii uhamishaji wowote wa programu kwa mhusika mwingine, na haki ya kuitumia, lazima ufuate sheria husika.

   a. **Programu iliyosakinishwa mapema kwenye kifaa.** Ikiwa ulipata programu iliyosakinishwa mapema kwenye kifaa (na kama pia ulipata toleo jipya kutoka kwa programu iliyosakinishwa mapema kwenye kifaa), unaweza kuhamisha leseni ya kutumia programu moja kwa moja kwa mtumiaji mwingine, kwa kutumia kifaa chenye leseni tu. Uhamishaji huo lazima ujumuishe programu na, ikiwa imetolewa na kifaa, lebo halali ya Windows inayojumuishwa ufunguo wa bidhaa. Kabla ya uhamishaji wowote ulioruhusiwa, mhusika yule mwingine lazima akubali kwamba mkataba huu unatumika kwa uhamishaji na utumiaji wa zanatepe.

   b. **Programu huru.** Ikiwa ulipata programu kama programu huru (na pia kama ulipata toleo jipya kutoka kwa programu uliyopata kama programu huru), unaweza kuhamisha programu kwenye kifaa kingine ambacho ni chako. Unaweza pia kuhamisha programu kwenye kifaa kinachomilikiwa na mtu mwingine ikiwa (i) wewe ndiye mtumiaji wa kwanza mwenye leseni ya programu na (ii) mtumiaji mpya anakubaliana na masharti ya makubaliano haya. Unaweza kutumia nakala chelezo tunayokuruhusu utengeneze au chombo ambacho programu ilikuja nayo ili kuhamisha programu. Kila wakati unapohamisha programu kwenye kifaa kipya, lazima uondoe programu kwenye kifaa cha kwanza. Huenda usiweze kuhamisha programu ya kushiriki leseni kati ya vifaa.

5. **Programu na Uamilishaji Ulioidhinishwa.** Umeidhinishwa kutumia programu hii ikiwa una leseni kamili tu na programu imeamilishwa vizuri na ufunguo halali wa bidhaa au na mbinu nyingine iliyoidhinishwa. Wakati unapounganisha Intaneti wakati unatumia programu, programu itawasiliana moja kwa moja na Microsoft au washirika wake ili kutekeleza uamilishaji ili kuhiusisha na kifaa fulani. Unaweza pia kuamilisha zanatepe wewe mwenyewe kwa Tovuti au simu. Kivyovyote vile, upitishaji wa maelezo mengine utatokea, na gharama za huduma za Intaneti, simu na SMS huenda zikatumika. Wakati wa Uamilishaji (au uamilishaji upya ambao unaweza kuanzishwa na mabadiliko ya vijenzi vya kifaa chako), huenda programu ikabainishwa kwamba tukio lililosakinishwa la programu ni bandia, halina leseni sahihi au linajumuisha mabadiliko yasiyoidhinishwa. Ikiwa uamilishaji utashindwa, programu itajaribu kujikarabati yenyewe kwa kubadilisha programu yoyote ya Microsoft iliyotatizwa na programu halisi ya Microsoft. Unaweza pia kupokea makumbusho ya kupata leseni halali ya programu. Uamilishaji sahihi hauthibitishi kwamba programu ni halisi au ina leseni sahihi.

Huruhusiwi kuruka au kulazimisha uamilishaji. Ili kusaidia kubainisha ikiwa programu ni halisi na kama una leseni sahihi, angalia (aka.ms/genuine). Visasisho vingine, usaidizi, na huduma nyingine huenda zikatolewa tu kwa watumiaji wenye programu halisi ya Microsoft.

6. **Visasisho.** Mara kwa mara programuhukagua visasisho vya mfumo na programu, na vipakuliwa na kuvisakinisha kwa niaba yako. Unaweza kupata visasisho kutoka kwa Microsoft au vyanzo vilivyoidhinishwa tu, na huenda Microsoft ikahitaji kusasisha mfumo wako ili kukupa visasisho hivyo. Kwa kukubali makubaliano haya, unakubali kupokea aina hizi za visasisho otomatiki bila ilani yoyoye ya ziada.

7. **Haki za kushusha Hadhi.** Ikiwa ulipata kifaa kutoka kwa mtengenezaji au msakinishaji mwenye toleo la Kitaalamu la Windows lililosakinishwa mapema, unaweza ukatumia toleo la Windows 8.1 Pro au Windows 7 Professional, lakini bora tu iwe Microsoft bado inatoa usaidizi wa toleo hilo la mapema, kama ilivyowekwa kwenye (aka.ms/windowslifecycle). Mkataba huu unatumika kwa utumizi wako wa matoleo ya awali. Kama toleo la awali linajumuisha vijenzi tofauti, masharti yoyote ya vijenzi hivyo katika mkataba ambao unaambatana na toleo la mapema hutumika kwa matumizi yako ya vijenzi kama hivyo. Mtengenezaji au msanidi, wala Microsoft, hawatawajibika kukupa matoleo ya awali. Lazima upate toleo la mapema kando, ambayo unaweza kulipishwa ada. Wakati wowote ule, unaweza kubadilisha toleo la awali na toleo ulilopata mapema.

8. **Vizuizi vya Kijiografia na Biasharanje.** Ikiwa programu yako imezuiwa ili itumiwe katika eneo fulani la kijiogrofia, basi unaweza kuamilisha programu katika eneo hilo tu. Lazima pia ufuate sheria na kanuni zote za biasharanje za kindani na kimataifa ambazo zinatumika kwa programu, ambayo hujumuisha vizuizi vya mwisho wa safari, watumiaji, na matumizi. Kwa maelezo zaidi kuhusu vizuizi vya kijiografia na biasharanje, tembelea (aka.ms/georestrict) na (aka.ms/exporting).

9. **Taratibu za Usaidizi na Kurejeshewa fedha.**

   a. **Kwa programu iliyosakinishwa mapema kwenye kifaa.** Kwa programu kijumla, wasiliana na mtengenezaji au msanidi wa kifaa kwa chaguo za usaidizi. Rejelea nambari ya auni iliyotolewa pamoja na zanatepe. Kwa visasisho na vipengele vya ziada vinavyopatikana moja kwa moja kutoka kwa Microsoft, huenda Microsoft ikatoa huduma kiasi ya usaidizi kwa programu yenye leseni sahihi kama ilivyofafanuliwa kwenye (aka.ms/mssupport). Ikiwa unatafuta fidia, wasiliana na mtengenezaji au msanidi ili kuamua sera yake ya fidia. Lazima uafikiane na sera hizo, ambayo huenda ikakuhitaji urejeshe programu na kifaa chote ambacho programu imesakinishwa ili kufidiwa.

   b. **Kwa programu iliyopatikana kutoka kwa muuzaji rejareja.** Microsoft hutoa huduma kiasi ya usaidizi kwa programu yenye leseni sahihi kama ilivyofafanuliwa kwenye (aka.ms/mssupport). Ikiwa ulinunua programu kutoka kwa muuzaji rejareja na unatafuta

fidia, na huwezi kupata moja mahali ambapo ulinunua programu, wasiliana na Microsoft kwa maelezo kuhusu sera ya urejeshaji ya Microsoft. Angalia (aka.ms/msoffices), au Marekani Kaskazini, piga simu (800) MICROSOFT au angalia (aka.ms/nareturns).

**10. Fungu linalofunga la Usuluhishi na Msamaha wa Kesi ya Pamoja ikiwa unaishi nchini (au Makao yako Makuu ya Biashara yako) Marekani.**

Tunatumani hatutakuwa na mzozo, lakini ikiwa utatokea, wewe na sisi tunakubali kujaribu kuutatua kwa njia isiyo rasmi kati ya siku 60. Ikiwa hatuwezi, wewe na sisi tunakubali **usuluhishi wa kufunga mbele ya Shirika la Usuluhishi la Marekani ("AAA") chini ya Sheria ya Usuluhishi ya Serikali ("FAA") na kutoshtaki mahakamani au mbele ya wakili au waamuzi.** Badala yake, msuluhishi asiye na upendeleo ataamua na uamuzi wa msuluhisi utakuwa wa mwisho isipokuwa kwa haki kidogo ya kukata rufaa chini ya FAA. **Mashtaka ya kesi za pamoja, usuluhishi wa kesi za pamoja, hatua binafsi za mwanasheria mkuu, na mashtaka yoyote ambapo mtu huwakilisha hayaruhusiwi. Hata pia kuchanganya mashtaka ya kibinafsi bila kibali cha wahusika wote.** "Sisi," "yetu," and "sisi" hujumuisha Microsoft, mtengenezaji wa kifaa, na msakinishaji wa programu.

**a.Mizozo inayoshughulikiwa—kila kitu isipokuwa IP.** Neno "mzozo" ni pana kama liwezavyo. Hujumuisha madai au ubishi wowote kati yako na mtengenezaji au msakinishaji, au wewe na Microsoft, kuhusiana na programu, bei yake, au makubaliano haya, chini ya nadharia yoyote ya kisheria ikiwa ni pamoja na mkataba, waranti, kosa la daawa, sheria, au masharti, **isipokuwa mizozo inayohusiana na utekelezaji au uhalali wa haki za rasilimali ya akili za mtoa leseni wako au mtoa leseni wetu.**

**b.Tuma kwanza barua yaIlani ya Mzozo.** Ikiwa una mzozo na waakilishi wetu wa huduma kwa wateja hawawezi kuitatua, tuma Ilani ya Mzozo kwa kutumia Barua ya Marekani kwa Mtengenezaji au msakinishaji, ATTN: LEGAL DEPARTMENT. Ikiwa mzozo wako unahusu Microsoft, itume kwa Microsoft Corporation, ATTN: LCA ARBITRATION, One Microsoft Way, Redmond, WA 98052-6399. Tueleze jina lako, anwani, jinsi ya kuwasiliana na wewe, tatizo ni nini, na ni nini unachokitaka. Fomu inapatikana kwenye (aka.ms/disputeform). Tutafanya hivyo pia ikiwa una mzozo na wewe. Baada ya siku 60, wewe au sisi tunaweza kuanzisha usuluhishi ikiwa mzozo haujatatuliwa.

**c. Chaguo la mahakama ya madai madogo.** Badala ya kutuma Ilani ya Mzozo, na ikiwa umefikia mahitaji ya mahakama, huenda ukatushtaki katika mahakama ya madai madogo katika nchi yako ya makazi (au ikiwa ni biashara, makao yako makuu ya biashara) au makao yetu makuu ya biashara-Kaunti ya Kingo, Washington Marekani ikiwa mzozo wako unahusu Microsoft. Tunatumaini utatuma barua ya Ilani ya Mzozo na kutoa siku 60 ili kujaribu kuutatua, lakini sio lazima kabla uende kwenye mahakama ya madai madogo.

**d. Utaratibu wa usuluhishi.** AAA itatekeleza usuluhishi wowote chini ya Sheria za Usuluhishi wa kibiashara (au ikiwa wewe ni mtu binafsi na unatumia programu kwa matumizi ya kibinafsi au ya nyumbani, au ikiwa thamani ya mzozo ni USD $ 75,000 au chini iwe wewe ni mtu binafsi au jinsi unavyotumia programu, Sheria zake za Usuluhishi wa Watumiaji). Kwa maelezo zaidi, angalia (aka.ms/adr) au piga simu 1-800-778-7879. Ili kuanzisha usuluhishi, wasilisha fomu inayopatikana kwenye (aka.ms/arbitration) kwa AAA; tuma nakala kwa mtengenezaji au msakinishaji (au kwa Microsoft ikiwa mzozo wako unahusisha Microsoft). Katika mzozo unaohusisha USD$ 25,000 au chini, usikilizaji wowote utakuwa kwa simu isipokuwa msuluhishi apate sababu nzuri ya kufanya usikilizaji wa uso kwa uso badala yake. Usikilizaji wowote wa uso kwa uso utafanyika katika nchi yako ya makazi (au ikiwa ni biashara, makao yako makuu ya biashara) au makao yetu makuu ya biashara-Kaunti ya Kingo, Washington Marekani ikiwa mzozo wako unahusu Microsoft. Chaguo ni lako. Msuluhishi huenda akatoa uamuzi sawa kwako wewe mtu binafsi kama vile mahakama inavyoweza kufanya. Huenda msuluhishi akatoa uamuzi wa kutangaza au amri ya kisheria kwako binafsi ili kurithisha madai yako binafsi..

**e.Ada na malipo ya usuluhishi.**

(i) **Mizozo inayohusisha USD$ 75,000 au chini.** Mtengenezaji au msakinishaji (au Microsoft ikiwa mzozo wako unahusisha Microsoft) itafidia mara moja ada yako ya kuwasilisha kesi na kulipa ada na gharama za AAA na msuluhishi. Ikiwa utakataa makubaliano yetu yaliyoandikwa mwisho yaliyotolewa kwako na msuluhishi mteule, mzozo wako utaenda kwa uamuzi wa mshauri (unaoitwa "uamuzi"), na mwamuzi akupe zaidi ya toleo hili lililoandikwa mwisho, mtengenezaji au msakinishaji (au Microsoft ikiwa mzozo wako unahusisha Microsoft): (1) italipa uamuzi mkuu au $1,000 USD; (2) italipa ada yako inayowezekana ya wakili, ikiwa ipo; na (3) kufidia gharama zozote (ikiwa ni pamoja na ada na ghrama za mshahidi mtaalamu) ambazo wakili wako alizipata kwa kuchunguza, kuandaa, na kufuatilia madai yako katika usuluhishi. Msuluhishi atabainisha kiasi isipokuwa ikiwa tutakubaliana nao.

(ii) **Mizozo inayohusisha zaidi ya USD$ 75,000.** Sheria za AAA zitasimamia malipo ya kuwasilisha kesi na ada na gharama za AAA na msuluhishi.

(iii) **Mizozo inayohusisha kiasi chochote.** Ikiwa utaanzisha usuluhishi hatutadai ada na gharama zetu za AAA au msuluhishi, au ada ada za kuwasilisha kesi tulizozifidia, isipokuwa msuljuhishi apate kwamba usuluhishi ni wa upuzi au uliletwa kwa lengo lisilofaa. Tukianzisha usuluhishi tutalipia ada na gharama zote za kuwasilisha kesi, za AAA na za msuluhishi. Hatutadai ada au gharama za wakili wetu kutoka kwako katika usuluhishi wowote. Ada na gharama hazihusiki katika kubainisha kiasi ambacho mzozo unahusisha.

f. **Lazima madai yawasilishwe ndani ya mwaka mmoja.** Wewe na sisi ni lazima tuwasilishe katika mahakama ya madai madogo au kusuluhisha madai au mizozo yoyote (isipokuwa mizozo ya raslimali ya akili — angalia Sehemu ya 10.a.) ndani ya mwaka mmoja kuanzia wakati ilipowasilishwa kwa mara ya kwanza. Kama sivyo, itazuiwa kabisa.

g. **Utenganishaji.** Ikiwa msamaha wa kesi ya pamoja utapatikana kuwa kinyume cha sheria au hauwezi kutekelezwa kwa sehemu zote au baadhi kwa mzozo, sehemu hizo hazitasuluhishwa bali zitaendelea hadi mahakamani, silizosalia zikiendelea katika usuluhishi. Ikiwa toleo lingine lolote la sehemu 10 litapatikana kuwa kinyume cha sheria au haliwezi kutekelezwa, toleo hilo litatenganishwa lakini sehemu iliyosalia ya 10 bado itatumika.

h. **Mzozo na sheria za AAA.** Makubaliano haya yanasimamia mizozo na Sheria za Usuluhishi za Kibiashara za AAA au Sheria za Usuluhishi za Watumiaji.

i. **Microsoft kama mhusika au mhusika mwingine anayefaidika.** Ikiwa Microsoft ni mtengenezaji wa kifaa au ikiwa ulipata programu kutoka kwa muuzaji rejareja, Microsoft ni muhusika katika makubaliano haya. Kama sivyo, Microsoft sio muhusika bali ni mhusika mwingine anayefaidika wa makubaliano yako na mtengenezaji au msakinishaji ya kutatua mizozo kupitia majadiliano na usuluhishi usio rasmi.

11. **Sheria Inayosimamia.** Sheria za jimbo au nchi unayoishi (au ikiwa ni biashara, mahali makao yako makuu ya biashara yapo) husimamia madai na mizozo yote inayohusiana na programu, bei yake, au makubaliano haya, ikiwa ni pamoja na ukiukaji wa madai ya mkataba na madai chini ya sheria za kuwalinda watumiaji za jimbo, sheria za ushindani usio wa haki, sheria za waranti, kujitajirisha kwa njia isio ya haki, na kosa la daawa, haijalishi mzozo wa kanuni za sheria, isipokuwa FAA husimamia matoleo yote yanayohusiana na usuluhishaji. Nchini Marekani, FAA husimamia matoleo yote yanayohusiana na usuluhishi.

12. **Haki za Watumiaji, Utofauti wa Kimaeneo.** Makubaliano haya hufafafaua haki nyingine za kisheria. Huenda ukawa na haki zingine, ikiwa ni pamoja haki za watumiaji, chin ya sheria za jimbo au nchi yako. Huenda pia kuwa na haki zinazohusiana na ulipotoa programu. Makubaliano haya hayabadilishi haki zile zingine ikiwa sheria za jimbo au nchi yako haziruhusu kufanya hivyo. Kwa mfano, ikiwa ulipata programu katika mojawapo ya maeneo yaliyo hapa chini, au sheria za lazima za nchi zinatumika, basi matoleo yafuatayo yanatumika kwako:

a. **Australia.** Marejeleo ya "Waranti yenye kikomo" ni marejeleo ya waranti ya moja kwa moja yaliyotolewa na Microsoft au mtengenezaji au msanidi. Waranti hii imetolewa kwa kuongezea haki na suluhisho zingine unazoweza kuwa nazo chini ya sheria, ikiwa ni pamoja na haki na suluhisho zako kulingana na hakikisho za kisheria chini ya Sheria ya Watumiaji ya Australia.

Katika sehemu hii, “bidhaa” hurejelea programu ambayo Microsoft au mtengenezaji au msakinishaji hutoa waranti ya moja kwa moja. Bidhaa zetu huja na uhakikisho ambao hauwezi kutenganishwa chini ya Sheria ya Watumiaji ya Australia. Una haki ya kubadilishiwa au kurejeshewa fedha kwa tatizo kubwa na fidia kwa hasara au uharibifu wowote unaoweza kubashiriwa. Pia una haki ya bidhaa kukarabatiwa au kubadilishwa ikiwa bidhaa haitakuwa na ubora unaokubaliwa na dosari sio dosari kubwa.

**b. Kanada.** Huenda ukakoma kupokea visasisho kwenye kifaa chako kwa kuzima ufikiaji wa Intaneti. Wakati utakapounganisha tena kwenye Intaneti, programu itaendelea kukagua na kusakinisha visasisho.

**c. Umoja wa Ulaya.** Kizuizi cha matumizi ya elimu katika Sehemu ya 13.d(i) hapa chini hakitumiki katika mamlaka yaliyoorodheshwa kwenye tovuti hii: (aka.ms/academicuse).

**d. Ujerumani na Austria.**

(i) **Waranti.** Programu yenye leseni halali itafanya kazi vizuri kama ilivyofafanuliwa katika nyenzo zozote za Microsoft ambazo zinaandamana na programu. Hata hivyo, mtengenezaji au msakinishaji, na Microsoft, haitoi hakikisho lolote la mkataba linalohusiana na programu yenye leseni.

(ii) **Kikomo cha Dhima.** Katika tukio la tabia ya kujua, utelekezaji mbaya, madai yanayohusiana na Sheria ya Dhima ya Bidhaa, na hata pia, katika tukio la kifo au majeraha ya kibinafsi au ya kimwili, mtengenezaji au msakinishaji, au Microsoft itawajibika kulingana na sheria.

Kulingana na sentensi iliyotangulia, mtengenezaji au msakinishaji, au Microsoft itawajibika tu kwa utelekezaji mdogo ikiwa mtengenezaji au msakinishaji au Microsoft itakuwa imekiuka majukumu kama hayo ya mkataba, uridhishaji ambao utawezesha utendakazi wa makubaliano haya, ukiukaji ambao utahatarisha lengo la makubaliano haya na makubaliano ambayo muhusika anaamini kabisa (yanayoitwa “majukumu makuu”). Katika hali nyingine za utekelezaji mdogo, mtengenezaji au msakinishaji au Microsoft haitawajibika kwa utelekezaji mdogo.

**e. Maeneo mengine.** Angalia (aka.ms/variations) kwa orodha ya sasa ya maeneo tofauti.

**13. Ilani za Ziada.**

**a. Matumizi ya mtandao, data na Intaneti.** Baadhi ya vipengele vya programu na huduma vilivyofikiwa kupitia programu vinaweza kuhitaji kifaa chako kifikie Intaneti. Ufikiaji na matumizi yako (pamoja na gharama) huenda yakategemea masharti ya makubaliano ya mtandao au mtoa huduma wako. Vipengele vingine vya programu vinaweza kukusaidia kufikia Itaneti kwa urahisi zaidi, lakini hesabu ya matumizi ya programu huenda ikawa tofauti na vipimo vya mtoa huduma wako. Daima unawajibika kwa (i) kufahamu na

kuafikiana na masharti ya mipango na makubaliano yako mwenyewe, na (ii) matatizo yoyote yanayotokana na kutumia au kufikia mitandao, ikiwa ni pamoja na mitandao ya umma/wazi. Unaweza kutumia programu kuunganisha kwenye mitandao, na kushiriki maelezo ya ufikiaji kuhusu mitandao hiyo, ikiwa tu una kibali cha kufanya hivyo.

**b. H.264/AVC na viwango oneshi vya MPEG-4 na viwango vya video vya VC-1.** Programu huenda ikajumuisha teknolojia ya usimbaji ya H.264/MPEG-4 AVC na/au VC-1. MPEG LA, L.L.C. inahitaji ilani hii:

BIDHAA HII INA LESENI CHINI YA LESENI ZA HATAZA ZA VC-1, NA MPEGE-4 SEHEMU YA 2 KWA MATUMIZI YA KIBINAFSI NA YASIYO YA KIBIASHARA KWA MTUMIAJI (i) KUSIMBUA VIDEO KULINGANA NA VIWANGO HAPA JUU ("VIWANGO VYA VIDEO") NA/AU (ii) KISIMBUA VIDEO YA AVC, VC-1 NA MPEG-4 SEHEMU YA 2 AMBAYO ILISIMBULIWA NA MTUMIAJI ANAYEHUSIKA KATIKA SHUGHULI YA KIBINAFSI NA ISIYO YA KIBIASHARA NA/AU ILIPATIKANA KUTOKA KWA MTOA VIDEO MWENYE LESENI YA KUTOA VIDEO KAMA HIYO. HAKUNA LESENI ILIYOPEANWA AU ITADOKEZWA KWA UTUMIZI MWINGINE WOWOTE. MAELEZO YA ZIADA YANAWEZA KUPATIKANA KUTOKA KWA MPEG LA, L.L.C. ANGALIA (AKA.MS/MPEGLA).

**c.Kinga dhidi ya programu mbaya.** Microsoft inajali kuhusu kulinda bidhaa yako dhidi ya programu mbaya. Programu itawasha kinga dhidi ya programu hasidi ikiwa ulinzi mwingine hautasakinishwa au umeisha muda wake. Ili kufanya hivyo, programu nyingine ya kuzuia programu hasidi italemazwa au italazimika kuondolewa.

**d. Matoleoyenye haki kiasi.** Ikiwa toleo la programu ulilopata limeteuliwa au limekusudiwa kwa matumizi fulani au yaliyozuiwa, basi unaweza kuitumia kama ilivyobainishwa. Huwezi kutumia matoleo kama hayo ya programu kwa shughuli za kibiashara, zisizo za faida, au kuzalisha mapato.

(i) **Elimu.** Kwa matumizi ya kielimu, lazima uwe mwanafunzi, mwadhiri au mfanyakazi wa taasisi ya elimu wakati wa ununuzi.

(ii) **Utathmini.** Kwa matumizi ya utathmini (au jaribio au kionjo), huwezi kuuza programu, kuitumia katika mazingira ya kuitumia moja kwa moja, au kuitumia baada ya kipindi cha utathmini. Bila kujali kitu chochote tofauti katika Mkataba huu, programu ya utathmini ya **imetolewa "KAMA ILIVYO" na hakuna waranti, ya kudokeza au ya kuelezea (ikiwa ni pamoja na Waranti yenye Kikomo), itatumika kwenye matoleo haya.**

(iii) **NFR.** Huwezi kuuza programu yenye alama ya "NFR" au "Sio ya Kuuza tena."

(iv) **Tangazo.** Unaweza kuchagua kutumia mwoneko awali, insider, beta au matoleo mengine ya mapema ya programu hii ("mioneko awali") ambayo Microsoft inaweza kutoa. Unaweza kutumia mioneko awali hadi tarehe ya mwisho ya

programu bora ufuate masharti yote ya mkataba huu. Mioneko awali ni ya majaribio na inaweza kuwa tofauti na toleo lililotolewa la kibiashara. Bila kujali kitu chochote tofauti katika Mkataba huu, **mioneko awali imetolewa "KAMA ILIVYO", na hakuna waranti, ya kudokeza au ya kuelezea (ikiwa ni pamoja na Waranti yenye Kikomo), itatumika kwenye matoleo haya**. **Kwa kusakinisha mioneko awali kwenye kifaa chako, unaweza kubatilisha au kuathiri waranti ya kifaa chako na huenda usiwe na haki ya kupata usaidizi kutoka kwa mtengenezaji wa kifaa chako au opereta wa mtandao, ikiwa anahusika.** Microsoft haijawabiki kwa uharibifu wowote unaosababishwa na wewe. Huenda Microsoft isitoe huduma za usaidizi kwa mioneko awali. Ukitoa maoni, mapendekezo au majibu mengine kwa Microsoft kuhusu mwoneko awali ("uwasilishi"), unaipa Microsoft na washirika wake haki za kutumia uwasilishi wako kwa njia yoyote ile na kwa lengo lolote lile.

**14. Mkataba Wote.** Makubaliano haya (pamoja na masharti ya leseni ya karatasi iliyochapishwa au masharti mengine yanayoandamana na nyongeza, visasisho, na huduma zozote za programu ambazo zimetolewa na mtengenezaji au msakinishaji, au Microsoft na ambazo unazozitumia), na masharti yaliyo kwenye viungo vya wavuti vilivyoorodheshwa katika makubaliano haya, ni makubaliano kamili ya programu na nyongeza, visasisho na huduma zingine kama hizo (isipokua mtengenezaji, au msakinishaji, au Microsoft iwe imetoa masharti mengine kama hayo na nyongeza, visasisho, na huduma kama hizo). Unaweza kuhakiki makubaliano haya baada ya programu kuendeshwa kwa kwenda kwenye (aka.ms/useterms) au kwenda kwenye Mipangilio - Mfumo - Kuhusu katika programu. Unaweza pia kupitia masharti katika viungo vyovyote katika makubaliano kwa kucharaza URL kwenye upau wa anwani wa kivinjari, na unakubali kufanya hivyo. Unakubali kwamba utasoma masharti haya kabla ya kutumia programu au huduma, ikiwa ni pamoja na masharti yoyote yaliyounganishwa. Unaelewa kwamba kwa kutumia programu na huduma, unaidhinisha makubaliano haya na masharti yaliyounganishwa. Pia kuna viungo vya maelezo katika makubaliano haya. Viungo vinavyojumuisha ilani na sheria za kufunga ni:

· Taarifa ya Faragha ya Microsoft (aka.ms/privacy)

· Makubaliano ya Huduma za Microsoft (aka.ms/msa)

· Masharti ya Leseni ya Adobe Flash Player (aka.ms/adobeflash)

**************************************************************************

**HAKUNA WARANTI**

PROGRAMU KWENYE KIFAA CHAKO (PAMOJA NA PROGRAMU) IMEPEWA LESEMA "KAMA ILIVYO." KWA UMBALI UNAORUHUSIWA NA SHERIA ZA ENEO LAKO, UBORA NA UTENDAKAZI

WA PROGRAMU UKO JUU YAKO. IWAPO ITAKUWA NA KASORO, UTAGHARIMIA GHARAMA YOTE YA KUIHUDUMIA AU KUIKARABATI. MTENGENEZAJI WA KIFAA AU MICROSOFT HAITOI WARANTI, HAKIKISHO, AU MASHARTI YOYOTE YA PROGRAMU. KWA UMBALI UNAORUHUSIWA CHINI YA SHERIA YA NCHI YAKO, MTENGENEZAJI NA MICROSOFT HAIJUMUISHI WARANTI NA MASHARTI YOTE YANAYOCHUKULIWA, IKIWA NI PAMOJA NA YALE YA UHAKIKISHO WA UUZAJI, UBORA, USAWA KWA LENGO FULANI NA KUTOKUKIUKA. HUENDA UKAWA NA HAKI ZA ZIADA ZA WATUMIAJI AU HAKIKISHO ZA KISHERIA CHINI YA SHERIA ZA NCHINI AMBAZO MASHARTI HAYA HAYAWEZI KUBADILISHA.

IKIWA SHERIA YA ENEO LAKO INATEKELEZA WARANTI, HAKIKISHO, AU MASHARTI HATA KAMA MAKUBALIANO HAYA HAYAFANYI HIVYO, MASHARTI YAKE YAMEZUIWA KWA SIKU 90 KUANZIA WAKATI MTUMIAJI WA KWANZA ULIPOPATA PROGRAMU. IKIWA MTENGENEZAJI AU MICROSOFT ITAKIUKA WARANTI, HAKIKISHO, AU MASHARTI KAMA HAYO, SULUHISHO LAKO LA PEKEE, KWA UTEUZI WA MTENGENEZAJI AU MICROSOFT, NI (I) KUKARABATI AU KUBADILISHA PROGRAMU BILA GHARAMA, AU (II) KUREJESHA PROGRAMU (AU KWA UTEUZI WAKE, KIFAA AMBACHO PROGRAMU IMESAKINISHWA) ILI KUFIDIWA KIWANGO KILICHOLIPWA, IKIWA KIPO. HAYA NI MAKUMBUSHO TU KWA UKIUKAJI WA WARANTI, HAKIKISHO, AU MASHARTI AMBAYO YANATEKELEZWA NA SHERIA ZA ENEO LAKO.

KWA UMBALI USIOKATAZWA NA SHERIA YA ENEO LAKO, IKIWA UNA MSINGI WOWOTE WA KUFIDIWA HASARA, UNAWEZA KUREJESHEWA NA MTENGENEZAJI AU MICROSOFT TU HASARA ZOZOTE ZA MOJA KWA MOJA KWA HADI KIWANGO ULICHOLIPIA PROGRAMU HIYO (AU USD$50 IKIWA ULIPATA PROGRAMU BILA GHARAMA YOYOTE). UNAKUBALI KUTOFIDIWA KWA HASARA ZOZOTE, IKIWA NI PAMOJA NA FAIDA ZILIZOPOTEA NA HASARA ZA MOJA KWA MOJA, ZINAZOTOKANA NA, MAALUM, ZISIZO ZA MOJA KWA MOJA, AU ZA BAHATI MBAYA, CHINI YA SEHEMU YOYOTE YA MAKUBALIANO HAYA AU CHINI YA NADHARIA YOYOTE. KIZUIZI HIKI HUTUMIKA KWA (I) KITU CHOCHOTE KINACHOHUSIANA NA MAKUBALIANO HAYA, PROGRAMU (PAMOJA NA PROGRAMU) KIFAA, HUDUMA, UHARIBIFU AU UPOTEZAJI WA DATA, KUSHINDWA KUPITISHA AU KUPOKEA DATA, MAUDHUI (PAMOJA NA MSIMBO) KWENYE TOVUTI ZA INTANETI ZA WAHUSIKA WENGINE AU PROGRAMU ZA WAHUSIKA WENGINE, NA (II) MADAI YA UKIUKAJI WA MKATABA, WARANTI, HAKIKISHO AU MASHARTI; DHIMA KALI, UTELEKEZAJI, AU KOSA LINGINE LA DAAWA; UKIUKAJI WA SHERIA NA MASHARTI; KUJITAJIRISHA KWA NJIA ISIO YA HAKI, AU CHINI YA NADHARIA NYINGINE YOYOTE.

VIZUZI VYA KUTENGWA KWA UHARIBIFU NA SULUHISHO KATIKA MAKUBALIANO HAYA HUTUMIKA HATA KAMA HUNA SULUHISHO LOLOTE (PROGRAMU IMEPEWA LESENI “KAMA ILIVYO”), IKIWA UKARABATI, UBADILISHAJI, AU FIDIA (IKIWA INAHITAJIKA NA SHERIA YA ENEO LAKO) HAIKUFIDII KABISA KWA HASARA ZOZOTE, IKIWA MTENGENEZAJI AU MICROSOFT ILIJUA AU INGEPASWA KUJUA KUHUSU UWEZEKANO WA HASARA, AU IKIWA SULUHISHO LITASHINDIKANA KUTEKELEZA LENGO LAKE MUHIMU.

Wasiliana na mtengezaji wa kifaa chako ili ubainishe ikiwa kifaa chako kinasimamiwa na waranti.